# KISWAHILI K.C.P.E

## SEHEMU YA KWANZA LUGHA

# MITIHANI YA UBASHIRI

MUDA: SAA MBI...

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA**
**SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO:**

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibia maswali .Kina maswali 50.

2. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika KARATASI YA MAJIBU na wala sio katika hiki cha maswali

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

3. Tumia penseli ya kawaida.

4. Hakikisha ya kwamba umeandika yafuatayo katika karatasi ya majibu.

   **NAMBA YAKO YA MTIHANI**
   **JINA LAKO**
   **JINA LA SHULE YAKO**

5. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani ( yaani namba ya shule, na zile namba tatu za mtahiniwa ) katika sehemu iliyitengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
6. Usitie alama zozote nje ya visanduku.

7. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usiikunje

8. Kwa kila swali 1 - 50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C, D, Nijibu MOJA tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.

9. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

   Mfano:
   23 `Tunakimbiana`maana yake ni?
   A. tunaogopana
   B. tunahepana
   C. tunasaidiana
   D. tunachukiana
   jibu sahihi ni B.
   Katika karatasi ya majibu:
   23. [A.] [B]. [C]. [D]

10. Chora kistari chako vizuri. kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku
11. Kwa kila swali. chora kistari katika kisanduku kimoja tu kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

## MTIHANI WA UBASHIRI WA KWANZA Saa 1 : dak 40

***Soma vifungu vifuatavyo vina nafasi 1– 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.***

Ni ______**1**______la kukera na ______ **2**______ kuona wana wetu wanalimbikiziwa majukumu ________**3**______ weza kuyamudu asilani. Hata hivyo wazazi wetu ______**4**______ kazi zao za nyumbani na kuwaachia vijakazi kule majumbani. Watoto sasa ndio ______**5**______ jukumu ______**6**_______ kuwalea wadogo wao pale ambapo baba na mama wote wako katika safu za kuajiriwa. ____**7**____weledi, ______**8**______.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | A. mambo | B. jambo | C. kitu | D. habari |
| **2.** | A. kukera | B. kukerekezwa | C. kukereketa | D. kukerana |
| **3.** | A. wasiyo | B. wasio | C. yasio | D. yasiyo |
| **4.** | A. wamekimbilia | B. wamekimbizwa | C. wamekimbia | D. wanayakimbia |
| **5.** | A. wametwikwa | B. wametweka | C. wametishwa | D. wametwezwa |
| **6.** | A. la | B. ya | C. cha | D. za |
| **7.** | A. chambilecho | B. vilevile | C. walivyosema | D. wazee |

**8.** A. Atangaye sana na jua hujua

B. Subira huvuta heri

C. Mwenda tezi na omo marejeo ni ngamani

D. Nyani haoni kundule

Wakati mabeberu __________**9**_______ hapa _______**10**______ Kenya, mipango ya elimu ya wasichana _______**11**________ sana. _______**12**_______ watu wengi walipenda ________**13**_______ watoto wao _______**14**_______. Lakini ilikuwa _______**15**______ kuwapatia elimu kamili.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **9.** | A. walikoingia | B. walipoingia | C. walipoondoka | D. waliondoka |
| **10.** | A. kwetu | B. yetu | C. mwetu | D. petu |
| **11.** | A. ilikuwa hafifu | B. walikuwa hafifu | C. haikuwa | D. kulikuwa hafifu |
| **12.** | A. ikiwa | B. ingawa | C. kwani | D. ajili |
| **13.** | A. kusoma | B. kuwasomea | C. kuwasomesha | D. kujisomea |
| **14.** | A. kike | B. wasichana | C. wakike | D. wa kike |
| **15.** | A. ngumu | B. gumu | C. vigumu | D. mgumu |

***Kutoka swali la 16 mpaka 30, chagua jibu lililo sahihi.***

**16.** Chagua wingi wa:
Hukuambiwa nakuhitaji wewe?
A. Hamkuambiwa tunawahitaji nyinyi?
B. Haukuambiwa tunawahitaji nyinyi?
C. Hamkuambiwa tunamhitaji nyinyi?
D. Hawakuambiwa tunawahitaji nyinyi?


**17.** Nomino ipi haijaambatanisha na ngeli sahihi?
A. Mbuzi ====> I – ZI
B. Moyo ====> U – ZI
X. Mvua ====> I – I
D. Mfugo ====> U – i

**18.** Piga mnada ni
A. Kuuza kwa bei ya juu.
B. Kuuza kwa bei ya rejareja.
C. Kuuza kwa kushindana bei.
D. Kuuza kwa kukopesha.

**19.** Chagua kundi lenye vihusishi pekee.
A. Isipokuwa, aghalabu, sembuse
B. Chini ya, kando ya, juu ya
C. Lo! kefule! salaale!
D. Ingawa, yarabii, tangu

**20.** Maneno yaliyopigwa mstari katika sentensi hii ni: <u>Yeye</u> alifanya mtihani <u>mgumu</u> upesi.
A. Kiwakilishi, kivumishi
B. Kiashiria, kiwakilishi
C. Kiwakilishi, kielezi
D. Kivumishi, kiwakilishi

**21.** Chagua methali isiyo na maana sawa na nyingine:
A. Mtegemea cha nduguye hufa maskini.
B. Mvumbika mbichi hula mbivu
C. Achanikaye kwenye mpini hafi njaa
D. Mgaagaa na upwa hali wali mkavu

**22.**


Mchoro huu unaonyesha:
A. Saa saba kasorobo
B. Saa saba na robo
C. Saa moja kasorobo
D. Saa tatu na dakika tano

**23.** Geuza katika kauli ya taarifa:
"Mwanangu, niletee kikoi kesho," mzazi alisema
A. Mzazi alimwamba mwanawe amletee kikoi kesho.
B. Mzazi alimwambia mwanawe niletee kikoi siku iliyofuata.
C. Mzazi alimwambia mwanangu amletee kikoi siku iliyotangulia.
D. Mzazi alimwomba mwanawe amletee kikoi siku iliyofuata.

**24.** Ni jibu lipi lenye maelezo yasiyo sahihi?
A. Kibofu huhifadhi mkojo tumboni.
B. Figo husafirisha damu mwilini.
C. Moyo husukuma damu mwilini.
D. Pafu husafisha hewa mwilini.

**25.** Onyesha sentensi yenye kielezi cha wakati
A. Asubuhi hiyo niliondoka kwetu
B. Maria atawasili alfajiri sana
C. Twende nyumbani upesi mno
D. Alikula chakula kingi sana.

**26.** Kanusha:
Utafiti uliofanywa uliridhisha wengi.
A. Utafiti uliofanywa haukuridhisha wengi.
B. Utafiti uliofanywa haujaridhisha wengi.
C. Utafiti usiofanywa haukuridhisha wengi.
D. Utafiti usiofanywa haujaridhisha wengi.

**27.** Neno "chakula" lina sauti ngapi
A. 7
B. 3
C. 6
D. 4

**28.** Mahali anapofungiwa mshatakiwa baada ya kupatikana na hatia
A. Kizimba
B. Seli
C. Rumande
D. Gerezani

**29.** Tegua kitendawili hiki
Afuma hana mshale.
A. Konokono
B. Nungunungu
C. Ndege
D. Samaki

**30.** Udogo wa sentensi hii ni
Ng'ombe alivunja kiti cha mzee.
A. Kigombe kilivunja kijiti cha kijizee.
B. Kigombe kilivunja kijikiti cha kizee.
C. Kigombe kilivunja kijiti cha kizee.
D. Kigombe alivunja kijikiti cha kijizee.

***Soma kifungu kifuatacho kasha jibu maswali 31 – 40***

Tatizo la ndoa za mapema zinazonasa wasichana wenye umri mdogo wanaofaa kuwa shuleni, ni tatizo linaloangamiza katika pembe tofauti kitaifa.

Maeneo mbalimbali nchini hutajwa wakati mwingi kuwa yameathiriwa zaidi na changamoto hii. Kinachofaa kutambulika ni kuwa maeneo mengi ambapo suala hili huwa limekithiri, huwa na kiwango kikubwa cha ukata.

Kama vile mkulima anavyokabiliana na magugu kwa kung'oa mizizi, hivi ndivyo jamii inafaa kukabiliana na tatizo hili sugu la ndoa na mimba za mapema kwa kutatua changamoto iliyo mzizini.

Umaskini ndio husukuma idadi kubwa ya wasichana wadogo, ambao baadhi yao huwa katika shule za msingi kuanza kujihusisha na tabia zinazowafanya kuishia kuwa wake za watu. Baadhi yao hulazimika kuolewa na wazee wenye umri unaotoshana na baba au hata mababu zao baada ya 'kuhimili', wasichana hao pia huhadaiwa kujiingiza katika hali hii kwa kununuliwa vitu ambavyo wao na wazazi hawana uwezo wa kugharamia.

Wengine huozwa kwa lazima kama njia ya kuwapatia jamaa zao mali kupitia kwa mahari inayotolewa. Dhana kuwa kuolewa pekee ni njia ya kuepuka ufukara, inafaa kukabiliwa vikali na jamii zilizo mashinani zifahamishwe hiyo ni dhana potovu iliyojaa upuzi. Msichana ambaye hauchishwa shule akiwa bado hajakamilisha elimu ya shule ya msingi, hataweza kujiinua kimaisha atakapoolewa.

Katika ulimwengu wa sasa, ni muhimu wake kwa waume wawe na uwezo wa kujitegemea wenyewe na isiwe eti msichana anaozwa bila kisomo kwa kudhani mume wake atakuwa akimtimizia mahitaji yake yote. Wazazi wanapaswa kufahamu bayana kuwa msichana anayepata elimu bora anaweza kuifaa sio tu jamii yake bali pia nchi nzima.

Idadi kubwa ya wazazi wanaowaoza watoto wao wa kike mapema, hufanya hivyo ili kujinufaisha na mahari yaliyotolewa, kwa kulalamika kuwa hawana njia nyingine ya kujiondoa katika lindi hili la umaskini. Mahari hayo ambayo wakati mwingi huwa tu mbuzi kadhaa hayawezi kulinganishwa na manufaa ya kudumu yanayoweza kupatikana ikiwa jamii itajikakamua kuhakikisha mtoto amepewa kile kidogo anachokihitaji kukamilisha masomo yake.

Kuna wanawake wengi ambao walilelewa katika jamii zenye umaskini mkubwa lakini wazazi wao walikuwa wenye busara wakivumilia matatizo yaliyowakumba bila kuzama katika tamaa ya kujitakia mali kwa haraka kupitia kwa mahari haramu.

Mahari hayo ni haramu kwa msingi kuwa huharibu mustakabali wa mtoto ambaye kikatiba ana haki zake. Sheria pia zipo za kulinda watoto kutokana na ndoa za mapema ilhali wazee wakongwe huzidi kuripotiwa kwenye vyombo vya habari wakijinyakulia wasichana ambao wameanza kubaleghe kama wake zao.

Jukumu la kulinda wasichana wanaotoka katika jamii maskini, si la serikali pekee bali wadau wote wanaohusika na masuala ya watoto wakiwemo walimu na viongozi wa kidini.

**31.** Tatizo la ndoa za mapema
A. Linasababishwa na wasichana wenye umri mdogo
B. Linapigiwa upatu na taifa zima
C. Linaathiriri wasichana wachanga nchini.
D. Linaathiri wasichana wote nchini.

**32.** Kipi kinachochangia hasa ndoa za mapema?
A. Umri mdogo wa wasichana
B. Mahari yanayotolewa na wazee
C. Taifa kuwa na changamoto nyingi
D. Hali kubwa ya umaskini

**33.** Maana ya "Mkulima anavyokabiliana na magugu kwa kung'oa mizizi," ni:
A. Kung'oa mizizi shambani
B. Kutatua chanzo asilia
C.. Wazee kulipa mahari
D. Wasichana kutopata mamba za mapema

**34.** Maana ya <u>'kuhimili'</u> ni
A. Kuwa mjamzito
B. Kuozwa mapema
C. Kubeba yaliyo mazito
D. Kushika mimba mapema

**35.** Chagua jibu sahihi kulingana na kifungu.
A. Ndoa za mapema ni tatizo la sehemu chache.
B. Wanawake walitoka jamii zenye umaskini hawamalizi masomo.
C. Jukumu la kuwalinda wasichana ni la serikali pekee.
D. Tamaa ya wazazi huchangia ndoa za mapema.

**36.** Si kweli kusema kuwa
A. Wazazi wengi hujinufaisha na mahari yanayotolewa
B. Wake kwa waume wana uwezo wa kujikimu wenyewe.
C. Msichana aliyeachishwa shule hujikimu kimaisha akiolewa
D. Msichana akipata elimu huwanufaisha wengi

**37.** Kulingana na aya ya mwisho jukumu la kulinda wasichana:
A. Linahitaji ushirikiano wa raia wote
B. Linahitaji ushirikiano wa serikali na walimu
C. Likahitaji ushirikiano wa viongozi wa kidini
D. Linahitaji ushirikiano wa wazazi pekee

**38.** Licha ya kuwa na sheria za kuwalinda watoto
A. Vyombo vya habari vinazidi kuongezeka
B. Serikali ina mkono mrefu sana
C. Mstakabali wao unazidi kuongezeka
D. Wasichana wanazidi kuozwa sana

**39.** Kulingana na mwandishi <u>mahari haramu</u> ni:-
A. Mahari yaliyokubalika
B. Mahari yasiyohalalishwa
C. Mahari yanayotolewa na wazee
D. Mahari yanayotolelewa na mbuzi

40. Chagua kichwa kifaacho zaidi kwa kifungu hiki
A. Mimba za watoto
B. Ndoa za mapema
C. Sheria za watoto
D. Elimu ya wasichana

***Soma taarifa hii kwa makini ksiha ujibu maswali 41 – 50***

Shule ya Songambele jijini Nairobi ilikuwa imekabiliwa na changamoto za kinidhamu miongoni mwa baadhi ya wanafunzi. Hulka na mitazamo ya waanfunzi kuhusu elimu ilikuwa mfano wa kuku kukokoneka huko akinyosha shingo kwenye kichaka alimojificha kicheche. Kicheche anayengojea kumla. Si wazazi, si wanafunzi, wote waliitemea mate mikakati ya kudumisha nidhamu na mbinu za adhabu zilizotumika shuleni humo.

Bwana Majadi, mshaurinasaha shuleni humo alikuwa katika njia panda baada ya kikao na wazazi wa bwamdogo Hamira na binti mdogo Kinyunya. Kiburi chao na kupuuza masomo kumbe kilitokana na kushiriki vileo walivyokuja navyo shuleni. Siku nne zilizopita wamefumaniwa maktabani katika hali ya kumwinamishia uso yeyote ambaye angewaona.

"Hawa ni watoto wadogo na huenda wanaigiza tu wayaonayo. Nia yao si unavyodhania labda iwe fikra zako ni hasi. Hakuna haja ya kuwaadhibu. Hiki ni kizazi dijitali." Wazazi walimkaba koo bwana Majadi akabaki amewakodolea macho. Aliyeakumbuka maisha ya utotoni kijijini Kegoye kaunti ya Vihiga.

Kijiji cha Kegoye kilikuwa na mengi ya kumchangamsha Majadi na wa rika lake. Wakati wa kuenda mtoni au machungani kulikuwa na michezo mingi tu: kupigana miereka, kucheza gololi, kukwea mitini na kandanda iliyopendwa na wengi. Mchezo uliotia fora sana ulikuwa ni mtelezo kwa kutumia mapande ya migomba kwenye miteremko iyomwagiwa maji au wakati wa mvua.

Kwa kweli mtoto achezapo, mbali na utangamano na kujikuza kiakili, kimwili na kihisia, hujisahaulisha kabisa na mazingira aliyomo. Kwa hiyo hata Majadi asingefahamu kuwa kaptura yake ilikuwa imechafuka na kusugulika makalioni wakati wa mtelezo. Aliona tu cha mtema kuni alipofika nyumbani.

"Umekuwa wapi?" Mama alimwuliza Majadi baada ya kumtazama sana.

"Nimetoka kwa mwalimu Musa Mukayaji. Nilikuwa nikipita tu akaniita na kunituma madukani Mbale nimnunulie gazeti, kisha mvua ikaanza kunyea." Majadi alimjibu mama yake kwa uso wa malaika.

"Kwa nini hakumtuma Mwanisa aliye mkubwa kwako?" Mama alimdadisi zaidi.

"Alikuwa mgonjwa kwa hivyo..."

Raap! Raap! Raap! Mama alimcharaza mgongoni.

"Ndio! Kumbe kutumwa dukani huchafua kaptura makalioni na hata kuzitoboa! Unafikiri nina pesa za kununua nyingine na sabuni ya kuzifulia? Utatembea vivyo hivyo na matundu hayo ndipo upate funzo."

Fulusi zilikuwa adimu. Jamaa nyingi hazikuwa na waliokuwa na mshahara mwisho wa mwezi. Kwa hivyo Majadi kununuliwa sare kulikuwa nadra sana sembuse mavazi? Kwa hivyo kaptura zilipopata matundu nyuma mfano wa donati mbili kuenda shuleni kulihitaji mbinu kabambe ili asionyeshe makalio. Kuwa kwake shuleni kukawa sawasawa na chatu anayelazimishwa kutambaa juu ya makaa ya moto. Aliupitisha muda mrefu ameketi.

Malezi ya vijana yalikuwa jukumu la wanajamii kwa jumla. Yeyote alikuwa huru kumwadhibu mtoto popote alipompata akifanya utundu. Mbali na kumwadhibu angefikisha ripoti nyumbani. Huko kungechochea adhabu ya pili. Baada ya adhabu hiyo, mzazi naye angefikisha ripoti shuleni. Huko angemwongezea mwanawe adhabu mbali na ile ya walimu. Hivyo basi ilimbidi kila kijana kuipiga msasa tabia yake.

Aidha, hata mtoni kulikuwa na mahali pa wasichana kuogea, kuogelea na kupiga mbizi. Mvulana yeyote angepatikana au angesingizia kisababu chochote cha kupitia eneo hilo angefedheheshwa na kuzomewa na kijiji kizima. Angedhihakiwa kwanza na wa rika lake na hasa wasichana kijijini. Jina lake lingetungiwa mizaha na nyimbo za masuto ambazo zingeimbwa shereheni. Wazazi wake wangeibeba tahayuri hiyo kote kote walikoenda. Ni nani angetaka kubeba mzigo huo?

Majadi alirudisha fikra zake kwa kisa cha Hamira na Kinyunya. Aliwaza kuwahusu wazazi wao. Aliwaza kuhusu kizazi cha vijana wa leo. Alitikisa kichwa akayaelekeza macho darini akayafumba.

41. Ni kweli kuwa shule ya Songambele
   A. Wazazi na wanafunzi walitetea viwango vya elimu na nidhamu
   B. Haikuwa na budi kuimarisha viwango vya elimu na nidhamu
   C. Wazazi na wanafunzi walizingatia viwango vya elimu na nidhamu
   D. Ilikuwa na budi kuimarisha viwango vya elimu na nidhamu

**42.** Maana ya kufananisha hulka ya wanafunzi na kicheche ni
   A. Kuhatarisha
   B. Kuzindusha
   C. Kuhamasisha
   D. Kutahadharisha

43. Kwa nini mwalimu Majadi alikuwa katika njia panda?
   A. Masimamo wake kuhusu nidhamu ulihitilifiana na wa wazazi
   B. Matukio ya Hamira na Kinyunya ilimwinamisha uso
   C. Waanfunzi walikunywa pombe na kukosa nidhamu
   D. Kiburi cha Hamira na Kinyunya kiliwalevya wakaacha ulimu

**44.** Kwa mujibu wa taarifa ni ukweli kuwa:

A. Wazazi wa leo wanahepa jukumu la malezi

B. Wazazai wa awali waliwadekeza wanao

C. Wazazi hushirikiana na walimu kudumisha nidhamu

D. Wazazi huwatetea watoto wao kwa haki

**45.** Chagua kundi la yote yaliyomvutia Majadi kijijini Kegoyo

A. Kukwea migomba, kabumbu, kushikana na kuangushana

B. Kuchunga mifugo, kucheza gololi, kupigana pambaja

C. Kukwea mitini, mtelezo, kupigana pambaja

D. Mtelezo, kushikana na kuangushana, kucheza gololi

**46.** Kulingana na taarifa ni jibu gani lisilo na faida ya motto kucheza?

A. Kujikuza kimwili na kihisia

B. Kujisahaulisha na mazingira

C. Kujikuza kimwili na kiakili

D. Kujikuza kiakili na kihisia

**47.** Majadi aliadhibiwa na mama kwa sababu gain hasa?

A. Alitumwa na mwalimu Musa Mukayaji

B. Alijua mama hakwa na peza za kununulia kaptura

C. Aliichafua na kuirarua kaptura yake

D. Alimcheza mama kayaya ya chini kwa chini

**48.** Kwa mujibu wa taarifa, mkondo wa adhabu mtoto alipokosa ulikuwa hivi:

A. Adhabu ya mwanajamii, mvyele, mdarisi na mvyele

B. Adhabu ya mwanajamii, mvyele na mdarisi, mhenga

C. Adhabu ya mdarisi na mhenga, mwanajamii, mvyele

D. Adhabu ya mdarisi, mwanajamii, mvyele na mhenga

**49.** <u>'Ni nani angetaka kuubeba mzigo huu'</u> Ni mzigo gani huo hasa kufuatana na taarifa?

A. Balaa ya kutungiwa nyimbo za masuto

B. Balaa ya kutengwa na marika

C. Balaa ya kutohudhuria sherehe

D. Balaa ya kuhamishwa na kijiji kizima

**50.** Ni funzo gani linaojitokeza katika habari hii:-

A. Adhabu kwa kizazi cha leo haifai kamwe

B. Ni muhimu wazazi kuwatetea wanao wakosapo

C. Kuchelea kuwadhibu vijana ni kujipalia makaa

D. Ni heri tuanze kuishi maisha ya zamani!